

**TARGETER WINGS**  
**KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI**  
**GREDI 1 - 2021**



**SHUGHULI ZA KISWAHILI  
KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA,  
KUSOMA KWA SAUTI**

**Jina .....**

**Jinsia:** Mvulana  **Msichana**

**Jina la shule .....**

## **1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 5)**

**Nitakusomea hadithi kisha nitakuuliza maswali. Kwa hivyo sikiliza kwa makini.**

Nilipoamka asubuhi nilimpata baba ameketi sebuleni akinywa chai. Nilimuamkua, "Shikamoo baba," Naye alinijibu, "Marahaba mwanangu." Baba alifurahi kuona kuwa nilijua kuamkua wakubwa wangu.

- a) Nilipoamka nilimpata nani?
- b) Alikuwa ameketi wapi?
- c) Nilifanya nini?
- d) Jibu la shikamoo ni nini?
- e) Kwa nini baba alifurahi?

## **KUSOMA KWA SAUTI**

**Soma hadithi hii kwa sauti.**

Mama alienda shambani kupalilia mimea aliyokuwa amepanda. Mama alikuwa amepanda mboga na mahindi. Mama alitumia jembe kupalilia. Baadaye mimea ilipokomaa aliivuna na kuipeleka sokoni kuuza. Mama alipata pesa za matumizi mengine.